Codutti Gianpaolo

# Historia fupi ya parokia Roho Mtakatifu pa Kitutu (Uvira, RDC)

Kwa kusherekea miaka 50 tangu kuundwa kwake

MIAKA 50

1967-2017



Édition Conforti, Bukavu, 2016

## YALIOMO

1. Utangulizi ........................................................................................ 3

2. Daftari ya Waxaveriano waliotumikia katika parokia ya Kitutu............................ 5

3. Mwanzo wa misioni.................................................................................... 8

4. Eneo la parokia, mwaka kwa mwaka (1970-2006)............................................. 10

5. Miaka kumi ya mwisho (2007-2016)................................................................ 19

6. Hadisi fupi ya diakonia zetu ........................................................................ 26

7. Waxaveriano na abbé waliokuwa Kitutu .......................................................... 31

8. Kwa kumaliza ........................................................................................... 34

# 1. UTANGULIZI



Kitutu, 1974

**Fasi na mitaa ya Kitutu**
Mji mkubwa katika mtaa wa Mwenga ndani ya ujamaa ya Wamuzimu, *Collectivité* inayo zunguukwa na mto Elila ndani ya mwitu *Equatori* kwenye barabara namba mbili ya taifa inayo elekea Kasongo.
Parokia hiyo inaundwa na mitaa miwili:

- Mtaa wa Shabunda
- Mtaa wa Mwenga.

Wote ni wa kabila mmoja ya Balega.

**Utangazaji wa Enjili mbele parokia kuundwa**

Kufuatana na maelezo ya watu, husema ya kwamba Wamissionari wa kwanza walipita Kitutu mwaka wa 1928 kutokea Pweto, katika jimbo la Katanga. Walipenda kusimama hapa Kitutu kwa kuunda Missioni, ila hapakuwa masikilizano kamili kati yao na mwami Longangi, ikasababisha wapite na kwenda kuunda Missioni ya kwanza pa Mulambula.

Tangu 1928 mpaka mwaka wa 1948, ilipoundwa Missioni ya Kamituga, Kitutu ilibaki chini ya maongozi ya Missioni ya Mulambula (iliongozwa na Pères Blancs).

Tangu mwaka wa 1948 mpaka 1967, Kitutu ilibaki chini ya maongozi ya Missioni ya Kamituga.

Kufuatana na maelezo ya Padri Festa Mario ndani ya kitabu chake *Ukumbusho wa miaka makumi matatu ya kuundwa Parokia ya Kitutu (1967-1997)*, Askofu Danilo Catarzi alipotoka Roma, tarehe 12/05/1965, aliahidia kwa Mwami Longangi kama kiisha miaka michache Kitutu itakua Parokia, kwa hiyo atayarishe: kiwanja, mawe na vifaa vingine kwa majengo. Tangu hapo, wakaaji wote walianza jitayarisha kwa kupokea Parokia mpya na Mapadri wapya wa kwanza.



Kitutu, 1974

**Mwendo wetu wa kuandika historia**

Katika historia ya Parokia ya Kitutu, tunafanya kifupi cha mambo mbalimbali na ya lazima kupitia:

01. Vitabu aliyoandika Padri Festa Mario, hasa:
    - Ukumbusho wa miaka makumi matatu ya Parokia (1967-1997).
    - Miaka miwili ya Parokia (l997-1999)
02. Tangu mwaka wa Elfu mbili (2000) mpaka sasa, kifupi za habari za kila mwaka, iliyo andikwa na Mapadri wengine wa Kitutu.

Hatuwezi andika vyote, ila kwa mistari michache ndani ya kitabu hiki tunafanya hadisi ya Parokia yetu ili tusisahau neema Mungu aliyotutendea.



Kitutu, 2008

## 2. DAFTARI YA WAXAVERIANO WALIOTUMIKIA KATIKA PAROKIA YA KITUTU


| Année | Arrivée | Départ | Nom | Charge |
|---|---|---|---|---|
| 1967 | 05.05.1967 | 01.09.1970 | Arrigoni P. Giuseppe | Curé |
| 1968 | 01.02.1968 | 01.03.1969 | Berton P. Angelo | Econome local |
| 1968 | 01.07.1968 | 01.07.1972 | Chiminazzo P. Attilio | Vicaire |
| 1969 | 01.07.1969 | 01.07.1974 | Chiminazzo P. Attilio | Econome local |
| 1969 | 01.07.1969 | 01.09.1969 | Marangoni P. Ezio | Vicaire |
| 1969 | 15.08.1969 | 01.05.1970 | Noris P. Italo | Vicaire |
| 1969 | 01.10.1969 | 15.08.1971 | Mazzuccato P. Antonio | Vicaire (fidei donum) |
| 1971 | 04.11.1970 | 30.08.1973 | Camorani P. Lorenzo | Curé |
| 1971 | 01.07.1971 | 01.09.1974 | Ferrari Fr. Angelo | Chargé des constructions |
| 1971 | 01.07.1971 | 30.06.1973 | Querzani P. Graziello | Vicaire |
| 1972 | 01.10.1972 | 01.09.1974 | Ballarin P. Lino | Vicaire |
| 1972 | 01.10.1973 | 01.09.1976 | Chiminazzo P. Attilio | Curé |
| 1972 | 25.12.1972 | 15.02.1976 | Rottini P. Aldo | Vicaire |
| 1973 | 01.07.1973 | 30.06.1976 | Nardo P. Riccardo | Vicaire |
| 1974 | 01.02.1974 | 10.09.1974 | De Mattia P. Pio | Vicaire |
| 1975 | 01.08.1975 | 05.01.1982 | Ferrari Fr. Angelo | Chargé des constructions |
| 1976 | 28.10.1976 | 25.09.1979 | Benedetti P. Silvano | Vicaire |
| 1976 | 06.01.1976 | 01.09.1981 | Dovigo P. Giuseppino | Curé |
| 1976 | 01.10.1976 | 30.06.1981 | Ferrari Fr. Angelo | Econome local |
| 1976 | 01.03.1976 | 30.06.1981 | Grigis P. Evasio | Vicaire |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 1980 | 05.01.1980 | 01.08.1984 | Colasuonno P. Nicola | Vicaire |
| 1981 | 17.01.1981 | 30.06.1984 | Cisco P. Giuseppe | Supérieur local |
| 1981 | 30.06.1981 | 01.09.1984 | Grigis P. Evasio | Curé |
| 1984 | 30.04.1984 | 30.11.1989 | Agostini P. Piergiorgio | Vicaire |
| 1984 | 01.07.1984 | 30.06.1986 | Cisco P. Giuseppe | Econome local |
| 1984 | 01.08.1984 | 30.05.1986 | Colasuonno P. Nicola | Curé |
| 1986 | 01.10.1986 | 30.06.1988 | Da Rold P. Sisto | Curé |
| 1987 | 01.02.1987 | 30.06.1990 | Raffaini P. Fiorenzo | Vicaire |
| 1988 | 01.10.1988 | 05.05.1996 | Valenti P. Giampietro | Vicaire |
| 1989 | 30.11.1989 | 14.07.1993 | Agostini P. Piergiorgio | Curé |
| 1992 | 01.11.1992 | 05.11.1996 | Berton P. Angelo | Vicaire |
| 1993 | 14.07.1993 | 11.05.1995 | Benedetti P. Silvano | Curé |
| 1995 | 11.05.1995 | 15.09.1996 | Benedetti P. Silvano | Vicaire |
| 1995 | 11.05.1995 | 07.12.1996 | Bon P. Renzo | Curé |
| 1995 | 13.03.1995 | 19.11.1996 | Marconi P. Dino | Vicaire |
| 1996 | 01.07.1996 | 10.06.1997 | Agostinis Pierfrancesco | Stage pastoral |
| 1996 | 01.07.1996 | 30.07.1997 | Festa P. Mario | Curé |
| 1996 | 01.07.1996 | 20.10.1997 | Tomasi P. Natalino | Vicaire |
| 1997 | 30.07.1997 | 29.09.2004 | Festa P. Mario | Vicaire |
| 1997 | 16.09.1997 | 30.04.1998 | Manzotti P. Antonino | Vicaire |
| 1997 | 10.03.1997 | 01.07.1999 | Rizzi P. Giuseppe | Econome local |
| 1997 | 20.10.1997 | 04.10.1999 | Tomasi P. Natalino | Curé |
| 1999 | 27.10.1999 | 01.06.2000 | Galli P. Giuseppe | Vicaire |
| 1999 | 15.11.1999 | 29.09.2004 | Rizzi P. Giuseppe | Curé |
| 2000 | 15.01.2000 | 01.04.2000 | Sciamanna P. Mario | Vicaire |
| 2000 | 06.12.2000 | 28.06.2005 | Turco P. Faustin | Vicaire |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 2001 | 01.09.2001 | 29.09.2004 | Rizzi P. Giuseppe | Econome local |
| 2004 | 29.09.2004 | 06.04.2005 | Festa P. Mario | Curé |
| 2004 | 29.09.2004 | 27.05.2006 | Rizzi P. Giuseppe | Vicaire |
| 2005 | 03.05.2005 | 05.05.2009 | Maran P. Paolo | Curé |
| 2005 | 21.06.2005 | 01.09.2006 | Rinaldi P. Pietro | Vicaire |
| 2006 | 05.12.2006 | 01.05.2008 | Jimenez Serrano P. Guillermo | Vicaire |
| 2006 | 23.06.2006 | 28.10.2008 | Mendoza Silva P. Roberto | Vicaire |
| 2006 | 19.11.2006 | 15.06.2009 | Simoncelli P. Giulio | Vicaire |
| 2008 | 06.06.2008 | 31.08.2010 | Olvera Gonzalez P. José Pedro | Vicaire |
| 2009 | 06.05.2009 | | Codutti P. Gianpaolo | Curé |
| 2009 | 05.11.2009 | 10.05.2010 | Pretel Ortiz P. Gerardo Ernesto | Vicaire |
| 2010 | 24.03.2010 | 27.04.2014 | Gonzalez Angulo P. Augustin | Vicaire |
| 2010 | 24.03.2010 | 26.03.2014 | Romano P. Antonio | Econome (fidei donum) |
| 2014 | 19.02.2014 | 21.10.2016 | Cibambo Rubibi P. Bernard | Econome local |
| 2014 | 19.02.2014 | | Harum P. Hieronimus | Vicaire |
| 2015 | 03.09.2015 | | Ndiwe Chiza Christophe | Stage pastoral |
| 2016 | 06.10.2016 | | Shadari Tutu P. Pauin | Econome local |

## 3. MWANZO WA MISIONI

Tangu tarehe 05/05/1967, Padri Arrigoni Joseph alitoka Kamituga kwa kuanza safari yake katika parokia mpya ya Kitutu. Kwa kupata mwangaza kamili juu ya uiio wake, tufuate barua yake aliyo andika:




"Nimefika kwa kubaki kwa lote katika missioni ya Kitutu tarehe 05/05/1967 kiisha kufanya safari yenyi kujaa magumu tele sababu ya njia na motokari ya zamani. Nilipo fika katika mgi wa kwanza wa Missioni yetu mpya, pa mto Kibe, motokari ikaharibika. Wakati nilikuwa nikijaribu kutafuta kosa lipo wapi, watu wakanifikia kunijulisha ya kuwa kando-kando kuna kijana mume wa somo la tano anayekuwa hatarini mwa kufa penye rabali ya metri makumi matano. Nikajiharikisha na nikamkuta akilala juu ya mlago, akiwa mahali ya nusu mufu, lakini alikuwa akisimulia kidogo. Alijaribu kusimama juu ya mulago, akakosewa nguvu, ndivyo nikashutama pembeni yake.

Tukasimulia naye ya kutosha. Mwisho nikamungamisha na nikamwomba kusali kwa ajili ya Missioni mpya. Naye akakubali ombi langu, akaniahidia ya kuwa wakati atafika nyumbani mwa Baba atabaki sikuzote pembeni yangu. Nikamega na kiisha dakika chache malaika huyu mdogo wa Missioni ya Kitutu akaruka mbinguni. Kwa kweli, alikuwa tunda la kwanza na msimamizi wa Missioni hii.

Sasa ni miaka ya kutosha tangu waamini wa Kitutu wamengojea ujio wa mtu wa Mungu. Mapokeo yalikuwa ya ajabu japo hayakuwa yenye kutayarishwa. Nimepangishwa mpaka mwezi wa saba 1968 katika nyumba ya udongo karibu na masomo. Nilikuwa mtu mpya katika sehemu hii ya nchi.

Sikujua kitu wala mtu mmoja. Mungu mwema akanitayarishia wasaidizi wangu watatu: Kakisingi Pontien, Byabele Dismas na Basubi Watukalusu wa Lugushwa, bila kusahahu Mwami Longangi Byemba na watu wengine wa mapenzi mema. Wale wote wakaniunga mikono wakibaki siku zote pembeni yangu wakiniongoza na mashauri yao mema". (Joseph Arrigoni)

**Mipango ya kazi ya mwanzo**
a) Mafundisho kuusu dini (Wakristu na wakatekista walikua wachache)
b) Maendeleo: Masomo na Makanisa.
Polepole, mwaka wa 1968, walifika mapadri wengine: P. Angelo Berton na P. Attilio Chiminazzo.





Kitutu, 1972

## 4. ENEO LA PAROKIA, MWAKA KWA MWAKA (1970-2006)

**1970**
Tangu mwaka huo, Eneo la Parokia ilikua ya kilometri mraba Elfu nne (4000 $km^2$), ambako wakatolika walikuwa Elfu sita mia tano (6500) kufuatana na ripoti ya Padri Festa Mario[1]. Mwaka huu wa 1970, Padri Arrigoni anaacha Parokia yake na kutumwa Uvira sababu ya maneno ya *kimbirikiti* kati yake na Abbé Mango. Yeye, Abbé Mango, akatumwa Bukavu.

**1971**
Mwaka huu ni ujio wa Padri Querzani aliye shurulika na matunzo ya wagonjwa wenye ukoma pa Kagelagela.

**1972**
Frera Angelo Ferrari anaanza majengo ya kanisa mpya (itamalizika katika mwaka wa 1974). Anaongoza majengo nyingine: majengo ya nyumba ya Mapadri na "Dispensaire" (leo bureau ya karani wa Parokia), nyumba ya



Kitutu, 1971 Querzani et Ferrari

---

[1] Cf. M. FESTA, *30ème anniversaire de la Paroisse de Kitutu*.

Masoeurs, Masomo ya msinji ya Kitutu centre (Somo nne na bureau moja). Wazazi, wakristu na wakubwa wa Collectivité walishirikiana kwa kwa msaada wa feza na kazi.

**1973**

Mwezi wa nane, siku makumi tatu na moja, na furaha tunapokea Masoeurs de la *Compagnie de Marie*: Maria Assuncion, Azuceno, Katsuva Madeleine, Mabruki na Justina. Watashurulika na *Dispensaire*, *Foyer social* na Katekezi.

**1974**

Tarehe 06/10/1974, kiisha miaka miwili ya ujenzi, Kanisa lilibarikiwa na Monseigneur Danilo Catarzi wakati wa Padri mkubwa Chiminazzo na wasaidizi wake, Rottini Aldo, Nardo Ricardo, Lino Ballarin na Frera Angelo Ferrari. Mapadri wengine walio shiriki mabarikio ni: Arrigoni, Berton, Ghirardi, Maragoni, Noris, Camorani, Mazzuccato, Querzani na Pio De Mattia (padri mpya). Wakati ule, Parokia ilikua na Diakonia sita: Kitutu centre, Mitobo, Maka, Kalukalu, Lugushwa na Kazuza. Pia tukawapokea waimizaji moja moja kwa kila Diakonia waliotayarishwa kwa kusaidia wakatekista wapya kwa kujua kutumia vitabu vipya na kuanza kuunda Mashirika. Mwezi wa nane mwaka 1974, kiisha mapatano ya Maaskofu, Pirigisha wa Kasongo na Catarzi wa Uvira, ndani ya Parokia ya Kitutu kuliongezeka Diakonia mbili: Diakonia ya Itula na Diakonia ya Zingu, zilizokuwa ndani ya Parokia ya Kalole Diocezi ya Kasongo. Polepole, Parokia ilifanya maendeleo ya Kirono kama vile ya Kimwili.

**1976**

Tunakumbuka ujio wa Mapadri wapya: Benedetti, Grigis na Dovigo aliye andika hadisi ya ukumbusho wa miaka kumi ya kuundwa Parokia ya Kitutu.

**1978**

Tulimaliza majengo ya *Dispensaire* mpya. Walio udumia kwenye *Dispensaire* hiyo walikuwa Masoeurs, wakisaidiwa na Laïque moja aliyeitwa Joséphine Agosti.

Kwa kuwasaidia watu kujuwa habari mbalimbali za Parokia, Mapadri waliunda Gazetti iliyoitwa Kamekemeke.

**1983**
Kwa maongozi ya Akina Baba Askofu Léonard Dhejju, tunaanza polepole hapa kwetu mafundisho juu ya kujibeba (hakuna msaada tena kwa Waongozi ao kwa Wakatekista).

**1988**
Tarehe 19/08 mwaka huu, hapa Kitutu kwa furaha tunakumbuka upadirisho wa mtoto wetu Alphonse Katindi Ramazani. Mwaka huu ni mwanzo wa kuundwa kundi la sala "Charismatique" ila mbele kulikuwako vikundi vingine, sawa vile: Waxaveri, Fraternité de Charles de Foucauld, Walejio. Vingine vilifika nyuma. Mwaka huu, tulipokea pia padri Jean-Pierre Valenti.

**1989**
Mapadri, pamoja na wakristu wa mapenzi mema, walijenga chumba cha michezo (Grande Salle), na vingine vinavyotumiwa kwa Ukatekumenato (*Centre Emmaüs)*, chumba cha kusomea vitabu (*Bibliothèque*) na karibu hapo *Atelier de soudure*, na pia waliendelea kujenga kituo cha kujifunzia kusoma, kushona na kuandika (*Foyer social*).

**1991**
Waxaveriano wanaacha parokia ya Mwenga: Kitutu inabaki Parokia moja tu ya Waxaveriano katika Mtaa wa Mwenga.

**1992**
Parokia ilifanya siku makumi mbili na tano ya kuundwa kwake. Ngambo ya majengo, tayari tulifanya hatua ya ujenzi wa masomo zimoja na wa makanisa moja moja za madiakonia. Ila magumu tunakutana nayo ni kwa ngambo ya maendeleo ya Kiroho:

- Ndoa za kikristu ni chache,
- Asili inatawala watu sana na
- Shirika moja moja ni zaifu.

**1995**
Kwa huzuni kubwa sana, katikati wa mwaka huu, Masera wetu wote wanatoka na kuiacha Parokia na kuendelesha kazi ya kitume fasi ingine.

**1996**

Mwezi wa kumi, tarehe 29, vita vilianza pa Bukavu na pale walimuuwa Askofu Munzihirwa. Tarehe 30/10/1996, padri Natalino Tomasi na séminariste Agostinis Pierre wanashurutishwa kutoka Luvungi na Baraka na, pahali pa kukimbia Ulaya, wanabaki wachungaji wa kondoo na kufika Kitutu.

**Wakati wa vita**

Tarehe 27/11/1996, mapadri waliombwa kukimbia (P. Bon Renzo, P. Festa Mario, P. Tomasi Natalino na Agostinis Pierfrancesco): walisindikizwa na wakristu mpaka Bakongo, kiisha waliendelea kwa Ngambwa, Kizuzu, Lolwe mpaka Kamituga (wanafika kisha siku 5 ya safari kwa miguu). Baada ya siku kumi, wakarudi Kitutu. Padri Bon anaenda ku matunzo Ulaya. Padri Natalino anafasiria matukio haya ya ukimbizi na vita:

"Mwezi wa kumi na moja, tumepata habari ya kwamba askari ya Kongo pamoja na vikundi vya jeshi la FAR (Forces Armées Rwandaises) wanakimbia kutoka Bukavu na wanakuja ngambo ya Kitutu. Walianza kukamata watu kwa kinguvu na kuomba makuta ili watu hawa wafunguliwe tena. Walipokuwa karibu na Kitutu, waongozi walitushauria kutoka kwa mda na kukimbia porini. Pale pale, tukaondoka usiku. Waongozi na vijana wanatusindikiza katika njia mwembamba n aza kufungana. Tulikuwa na tala moja ndogo kwa kutuangazia. Wakristu wamoja wanatusalimia ila hawajui bado yenye inatokea. Nyuma yetu, kuna wale wanatuambia: *Wale wajambazi wanawatafuta!* Halafu wasaidizi wetu wanakamata mkono wetu na kutubeba kwa haraka mda wa saa nzima mbele ya kufichama ndani ya nyumba ya mkristu moja, kwenye tunabaki mchana mzima. Kesho yake tunafika Kamituga: wanatuambia kama missioni wa Kitutu iliporwa na jeshi hutu na ya kwamba zamu ya nyumba ya masoeurs aliuawa. Tunashukuru waliokubali kubaki katika misioni ya Kitutu: mwongozi Lunanga Witangila, zamu Ibanze Raphael, mama Mzee, Wasolu Michel na wengine waliotia maisha yao katika hatari kwa kutimiza mapashwa yao. Wakaaji wote wakakimbia porini. Kisha siku chache, tunarudi Kitutu kwa kutayarisha Noeli. Yesu alikuja kutuletea amani kwa ajili ya wakristu wetu". (Natalino TOMASI, « L'ultimo suo racconto », *Missionari Saveriani*, décembre 1999, p. 8).

**1997**

Japo vita, parokia haikubaki wazi bila padri kuwako. Mapadri wakaendelea na utumishi wao japo magumu. Kwa juhudi ya pekee, waliweza pia kuwatembelea wakristu wa Diakonia za mbali.

**1998**

Jamaa la mapadri ilibaki kama hivi: P. Tomasi Natalino, Curé; P. Festa Mario, Vicaire; P. Rizzi Pino, Econome local na P. Manzotti Antonino, kwa mda. Mwaka huu ulianza katika hali ya mashaka, hapakuwa na Misa kubwa siku za Mungu. Watu walianza kukimbia miji, wakihama na kwenda nafasi zingine (Kamituga, Bukavu...) ila Mapadri walizidi kubaki na kutia watu moyo wakipiga kengele ya Misa: hata waliokuwa porini walikuwa wakisikiliza kengele ya Missioni na wakatiwa matumaini. Tarehe 09/08/1998, askari wanaingia pa 20h na pa 22h, wakiwafungia mapadri katika chumba moja, wakiwatiisha na bunduki wakisema kama watauwawa. Mwisho, wakapora pesa na mali ya parokia.

Tarehe 28/08/1998: mauaji wa Kasika. Wakimbizi wa Kasika wanafika mpaka Kitutu na wakaaji walianza kusema: “Hata huku ile mauaji inaweza fanyika”. Tulichanga woga na imani. Padri Natalino anaandika katika buku yake: “Mungu anatuita tutakase mwenendo wetu, tuishi katika kuheshimiana na tuchukue msalaba tukiaminia ufufuko wa Yesu. Ee Mungu, utuletee amani. Uwazidishie wakristu wetu imani. Utujalie juhudi na nguvu katika majaribu”.

Padri Natalino anaandika:
*Tarehe 24/09/1998, kamanda ya jeshi anatafuta kuua askari wake mbele ya watu kwani alipiga lisasi, akilewa, mpaka kuua kijana moja ya Bazee. Mbele ya watu wote, baba ya kijana marehemu anapaliza sauti: “Musimwuue yule askari. Mungu tu anatuhukumu. Mmsamehe”. Ule baba alitoa ushuhuda bora katika majaribu: ni mkatekista wetu.*

**1999**
Kwa mda mrefu, Mapadri walibaki wawili: Festa alipokwenda mapumziko, alizuilika kurudi haraka sababu ya vita. Aliweza kurudi tu kisha miezi tano.
Kwa huzuni kubwa, tarehe 04/10/1999 pa saa moja na nusu, tulipokea habari ya kifo cha Padri Natalino Tomasi ku hospitali kuu pa Bukavu, alipoenda kutunzwa magonjwa ya mshipa (hernie). Aliondoka hapa Kitutu tarehe 23/09/1999 na Avion ya Padri Denis, na siku ileile alipasuliwa, lakini mambo hayakuendeka. Alizikwa pa Bukavu, tarehe 05/10/1999, kunako Shamba la wafu la Waxaveriano (Panzi).
Pahali pake, padri Pino Rizzi aligeuka kuwa Padri mkubwa na mwezi wa kumi, Padri Giuseppe Galli anafika kwa kusaidia, kutoka Panzi. Tunakumbuka ya kwamba vita vilidumu sana mwaka wa 1999: watu waliishi mda mrefu porini (zaidi ya miezi sita) ila Mapadri walibaki mjini.

**2000**
Mwezi wa kumi na mbili, siku sita ya mwezi, Padri Faustin Turco anafika Kitutu, na Padri Galli anarudi Bukavu ila tulibaki katika wasiwasi ya vita, kwa kuunguzwa nyumba na kuuwawa kwa wakaaji kama vile Mukandilwa Sawabita. Tarehe 19/12/2000, askari wa RCD walipigana na Mai-mai pa Kakolokelwa. Watu kumi wakafa. Padri Pino akalazimishwa na askari kwenda kuchukua walioumizwa. Na juhudi kubwa, akaenda na akaona maiti ya mtoto alieuawa. Kwa kuwa alikuwa akivaa viupa viunoni, askari walikuwa wakiendelea kumpiga maiti. Baadaye padri Pino akaandika “Barua kwa kijana wetu mai-mai” kwa kuonyesha ginsi tunahitaji amani na maongozi wa kweli.

**2001**
Mapadri walikuwa watatu (P. Pino Rizzi, P. Faustin Turco na P. Mario Festa). Japo vita kuendelea kuwa kali, jamaa la Mapadri waliendelea kwa kuwasaidia watu wakishirikiana pamoja na Waongozi na wengine watu wa mapenzi mema. Katika mango wa kuongoza vijana, Padri Faustin Turco aliunda kundi la Wito.

**2002**

Kundi la Mapadri lilibaki vilevile (Watatu, mpaka mwaka wa 2005). Kwa jumla, mwaka huu mashariki mwa Kongo na kwa upekee Kitutu, vikundi mbalimbali vya wapiganaji viliendelea kutatiza wakaaji, ila RCD, kundi moja kati ya hizo, ilitafuta kutawala zingine kundi na kuchukua Uongozi. Tarehe 28/05/2002, raia 8 wakauawa na Interhamwes waliongia katika Collectivité ya Kitutu. Kisha, tangu tarehe 25.08.2002 mpaka 04.09.2002, mjini wa Kitutu ilikamatwa na Interhamwes pamoja na kundi la Mai-Mai. Tarehe 25/12/2002, katikati ya misa ya Noeli, kisha matoleo, wajambazi wakaanza kupiga bunduki… wakristu wakatoka nje na wakakimbia. Misa haikuendelea tena: habari ya Noeli inatia wivu kwa wasiopenda amani.

**2003**



Vita viliendelea hapa na pale ila maendeleo hayakukoma. Kwa ngambo ya masomo, tuliopokea msaada kutoka jamaa ya marehemu P. Natalino Tomasi na wengine watu: mapadri waliweza kutengeneza rnasomo ya msingi ya Twabenga, sababu tangu mwaka wa 1989, masomo hii ilichangwa pamoia na Kibilila, kwa kukosa majengo mazuri. Kwa sasa masomo hiyo inaitwa "E.P Twabenga P. Natalino".

Katika mwaka ule, ilipoonekana kama mkondo (*section*) wa hesabu, kunako masomo ya secondari ya Elila, haukufaulu kutoa Diplôme d'Etat, waliongeza mkondo wa kipedagogia.

Tarehe 05/01/2003, alipigwa na kuuwawa na Waaskari, bwana Masumbuko Lushike Pierre (mume wa Bisobekwa Celina). Alipotafuta kutetea kifo hicho, kunako tarehe 07/02/2003, Padri Faustin alifukuzwa na mkubwa wa Waaskari,

Commandant Bora Uzima, pamoia na Administrateur wa Mwenga wa wakati ule. Alibaki nje ya Parokia yake mda siku makumi saba.
Kwa mwaka huu, tokeo lingine kubwa ni kumpokea kwa furaha Askofu mpya wa Uvira, Tafunga Mbayo Jean-Pierre, aliyeleta tulizo na matumaini na kuwapa Wakristu moyo kulingana na vita.
Tarehe 01 na 08, mwezi wa sita, roquettes mbili walianguka ndani ya lupango la mapadri wa Kitutu: kwa neema hakuna mwenye aliumizwa, ila gari ilibomoka.

**2004**
Hakuna mabadiriko katika jamaa la mapadri. Tunakumbuka mwezi wa kwanza masimulizi kati ya RCD na Mai-Mai (Vikundi vya kisiasa) ndiyo mwanzo wa mapatano. Mwezi wa tano, mapatano kamili ikasherekewa pamoja tarehe 17/05/2004.

**2005**
Mwaka huu tulimpokea Padri Paulo Maran. Padri Mario Festa, tarehe 06.04.2005, anatuaga na anaendelea utumishi pa Kavimvira, kisha miaka kenda tangu amefika Kitutu:

> *"Naenda na furaha kwa kuwa nimeonana na rafiki wengi huku Kitutu. Naenda pia na sikitiko kwa wema nilishindwa kuutenda. Naenda zaidi nikimwaminia Mungu anayetimiza, sasa ao baadaye, ahadi zake. Mbali na macho, ila karibu ya moyo!"*

Kwa msaada tuliopokea toka Ulaya kwa mtu moja wa mapenzi mema, Padri Paulo Maran, Faustin Turco, Pino Rizzi na laïc mmoja, Antonio Paggi, walikerebisha masomo zetu za Kitutu centre na, mwezi wa kenda, paa ya nyumba ya Mapadri.
Tarehe 05/03/2005, tulipokea habari ya kifo kwa rafla cha mwami wa Collectivité ya Wamuzimu Longangi Ali Byemba Justin pa Bukavu. Maziko ilifanyika pa Kitutu, na Ibada ilisomwa na Padri Pino Rizzi.
Tarehe 03/05/2005, Padri Maran aligeuka kuwa Curé, Pino Rizzi, kuwa mlinda Azina na Faustin Turco Vicaire. Baadaye tarehe, 26/06/2005, Padri Faustin alihamishwa Bukavu na kugombolewa na Padri Pietro Rinaldi.

**2006**

Mapadri walikuwa: P. Paulo Maran, P. Pino Rizzi na P. Pietro Rinaldi.

Hatuwezi kumsahau Padri wetu Pino Rizzi aliye kwenda Bukavu kwa matunzo na Padri Pietro Rinaldi aliye kwenda Ulaya kwa kilio cha Baba yake: wote wawili hawakurudi tena Kitutu.

Waligombolewa na Padri Memo (Jimenez Guillermo), Padri Mendoza Roberto Carlos na Giulio Simocelli.

Katika mwaka huu, kuona kama Parokia ni kubwa, Mapadri walikusudia kugawanya Parokia kwa secteur nne.

1. Secteur Nord, inayo Diakonia nne : Kibe, Makito, Sugulu na Mitobo.
2. Secteur Centre, inayo Diakonia sita : Kitutu, Milima, Byonga, Maka, Iwiwi na Tukenga.
3. Seteur Sud, inayo Diakonia tano: Kazuza, Kagelagela, Itula, Zingu na Kitindi.
4. Secteur Bassin d'Elila, inayo Diakonia sita: Mela, Kakemenge, Butetegele, Lugushwa, Kabikokole na Bonde.



Centre de santé « Busakizi-Kitutu », 2008

## 5. MIAKA KUMI YA MWISHO (2007-2016)

**2007**
Mwaka ulianza na Mapadri: P. Paulo Maran, Curé, Mendoza Roberto Carlos, mlinda azina, Padri Mémo, msimamizi wa vijana na wa kundi la Uwito, Padri Giulio Simoncelli aliyeshurulika vikundi vingine.
Wanamemba wa kundi la wito wanaanza kwenda katika Propédeutique: kijana Alamo Pona Dominique alianza Propédetique, matayarisho ya kusoma kipadiri. Nyuma yake, kijana Jean-Baptiste Mulonda Lweku alifuata njia ile.
Kwa furaha kubwa tena, tanapokea kwa mara ya pili, Akina Baba Askofu Tafunga Mbayo Jean-Pierre.
Kiisha kurudi kwake Askofu, na kwa maombi ya Padri Paolo Maran, tulifungua Shirika *Mamma della Pace* iliyosimamiwa na wamama: Mama Léontine Nyamwenda, Mama Françoise na mama Furaha.
Ukomo wa shirika hilo ni kupokea na kushurulika kwa ajili ya watoto mayatima watakao udumiwa ndani ya nyumba ya Masoeurs. Kwa bahati mbaya, walifunga milango na kurudi kwao kwa sababu ya matatizo mbalimbali.

**2008**
Mapadri walikuwa: Padri Paolo Maran, Padri Roberto Carlos, Padri Simoncelli Giulio na Padri Pedro Olvera Gonzalez aliyefika kwetu kwa mara ya kwanza, tarehe 06/06/2008 kwa kugomboa Padri Mémo.


Kitindi, 2008

Mwaka huu UNICEF ilipenda kuanzisha masomo ya Watoto “3 ans - 5 ans” (*Espérance communauté d’éveil*), lakini mambo hayakuendeka.

**2009**

Jamaa la Mapadri liliongezeka kwa ujio wa Padri Codutti Gianpaolo aliyefika mwezi wa kwanza na padri Gerardo Pretel aliyekuja tarehe 05/11/2009. Kwa juhudi na kwa msaada ya Mapadri wenzake, Padri Paolo Maran alifanya taswira (*Croquis*) mpya ya Eneo ya Parokia « Kitutu centre » bila kusahahu Baba chef de collectivité a.i., Godefroid Byembe Luzuza, aliyetuunga mikono kwa kazi hiyo nzito. Kiisha kazi hiyo, Padri Maran alihamishwa, mwezi wa tano, na kwenda nafasi zingine, na Giulio mwezi wa sita naye alituacha.

Kwa kusaidia Mapadri, walituma laic mmoja, bwana Francesco Bazzoli mda wa miezi mitano. Tarehe 09 mpaka 11/09/2009, ndani ya shaari kuu ya Parokia, tulikusudia yafuatayo:

1. Kwa kila shauri, kila Diakonia kutuma wajumbe tatu yaani: Mwongozi mmoja na wajumbe wengine wawili kati yao mwanamke mmoja,
2. Kwa kila shauri, wausika wanapashwa kuleta michango yao,
3. Kila Diakonia inanashwa saidia Parokia na nusu ya mia (50%) ya matoleo yao,
4. Ukatekumenato, Komunio ya kwanza ya Watoto, itaanza kufuatwa, Watoto wakiwa na Umri ya iniaka nane.

Katika mwaka huu, mwezi wa sita, kwa huzuni kubwa Parokia ikampoteza karani wake bwana Kika Louis (aliyeitwa pia *Padiri*) kwa magonjwa ya *Diabète* na akagombolewa na Kakondja Kyalondawa Dieudonné, mwezi wa saba, siku 29.

**2010**

Mwaka ulionekana kuanza na wasiwasi. Japo hiyo utumishi katika Parokia haukukoma. Kuona shida katika Diakonia zimoja, ndani ya shauri kuu la Parokia, mwezi wa pili, Diakonia zimoja kwa mapenzi mema, walisaidia wenzao waliopatwa na shida kwa misaada mbalimbali (kipesa: 97.350FC na vifaa vingine vingi...).



Milima, 2008

Kwa mshangao mkubwa, na kwa rafla, tarehe 01/03/2010, kilalo juu ya mto Elila ilitumbukia ndani ya mto, na juu ya kilalo Gari moja kubwa ambamo ilikua nachukua watu na vifaa mbalimbali... ginsi tulivyo ambiwa, watu kenda walizama na watatu waliokolewa. Tangu siku ile, Kitutu ilibaki bila Gari. Watu walianza kuvuka kwenye mitumbu. Vitu vikapandishwa bei. Kiisha mwaka moja kilalo kilijengwa upya.
Mwezi wa tatu tuliwapokea Mapadri wawili: Padri Augustin Gonzalez (Mxaveriano) na Don Antonio Romano (abbé ya Diocèse ya Salerno, Italie). Mwezi wa nane, Baba yake Antonio, Pellegrino na kaka yake Giuseppe walifika Kitutu na walitujengea "four" ya kuchomea. Mwezi wa kenda, Mganga wa magonjwa ya ngozi na Chirurgien, Andrea Galla, alifika kusaidia kwenye kituo cha afia Busakizi.



Sugulu, 2008

**2011**

Ulianza na Mapadri: P. Gianpaolo Codutti, P. Don Antonio Romano na P. Augustin Gonzalez. Mwaka huu, kama mwaka uliopita, wasiwasi ulizidi katika Parokia yote. Ndani ya Diakonia ya Sugulu, jambo kubwa ni la wizi ndani ya nyuwba za wakaaji na kuchoma zingine. Lakustaajabia ni kufikia kumpeleka Mwongozi Alexandre Faliala porini na kuomba kiasi ya dolari Elfu moja (1000) kama vile malipo kwa kufunguliwa kwake. Japo matatizo haya yote, Mapadri waliendelea na utumishi wao. Kwa ngambo

ya maendeleo, walimaliza Masomo ya secondari ya Kanguli "Beltrame" pa Itula.
Tarehe 11 mpaka 25/05, tulimpokea Padri Riccardo Nardo, Exorciste, kwa kusaidia wakristu wanaogonjwa (Mwili na Roho). Padri Vignato pia alifika kwa mda kwa kusaidia.
Tarehe 23/10/2011, tulisherekea kutajwa kwake kuwa mtakatifu Guido Maria Conforti mwanzilishi wa jamaa la Waxaveriano ulimwenguni.

**2012**

Kama vile mwaka wa 2011, Mapadri walikuwa walewale. Mwaka huu ni wa pekee, kwa ajili ya ukumbusho wa miaka makumi tano tangu kuundwa Diocèzi yetu ya Uvira (mwaliko wa sala kwa ajili ya wote waliojitolea kimwili na kiroho). Hapa Kitutu, ukumbusho ule ulifanyika tarehe 27/05/2012, sikukuu ya Pentecoste, na Misa kubwa iliongozwa na Arkiaskofu wa Bukavu Maroy Rusengo François-Xavier, kwa mda msimamizi wa Jimbo la Uvira.
Mwezi wa nane tuliwapokea Anna, dada wa Don Antonio, na marafiki yake tatu, pia Renato Fochesato, maçon, aliyesiadia kwa ujenzi wa misingi ya Masomo ya Kibilila 2.
Kwa heri Baba Wabesha Eugène, msimamizi wa kundi la *Renouveau Charismatique* katika Parokia: alikufa kwa kifo cha rafla, tarehe 24/08/2012. Tarehe 11/12/2012, ndani ya Parokia tulianza mwaka wa imani uliotangazwa na Papa Benedicto XVI. Majilio ilipofika, kwa matembezi ndani ya Diakonia, tulisaidiwa na Padri Willy Nkumbo kutoka Bukavu.



Kakemenge, 2008

**2013**
Mwaka ulifanana kuanza na amani hapa Kitutu. Jamaa la Mapadri lilikua lilelile. Mzee Pellegrino alifika kujenga “Tank” ya maji kunako kituo cha afia Busakizi. Tulipoona uzaifu unaingia katika Diakonia zetu, wakati wa Paska na kiisha Paska, tuliitisha mkutano ya siku mbili na ikakusudiwa kama hivi: kila secteur kuimiza wauzuriaji wake juu ya *Shirika Amka*, *Katekismo*, *Sala ya kusadiki* na maisha ya Yesu. Tulisaidiwa pia na Padri Faustin Turco.
Tarehe 03/06/2013, njiani kwa kwenda Bukavu, Mapadri Gianpaolo Codutti, Don Antonio Romano na Padri Augustin Gonzalez pamoja na wafanya kazi wamoja, walinyanyaswa na wabandits wakivalia stare za kijeshi.
Tarehe 19/08/2013, kwa safari ya kwenda kutwaaa Padri Antonio pa Bukavu, tendo lilelile likafanyika mara ya pili na nafasi ileile, mara hiyo Mapadri walikuwa wawili (Gianpaolo na Augustino) na wateja wengine.
Tarehe 15/10/2013, kama vile ndoto, kwa shangwe kubwa tulipokea habari ya kutajwa kwake Baba Sébastiano Muyengo Mulombe kama vile Askofu wa jimbo letu la Uvira.
Tarehe 15/11/2013, tuliwapokea kwa furaha kutoka Bukavu wa Laiques Consacrées wawili: Christine na Marie-Jeanne, mmoja mganga na mwingine mwalimu. Wote waliishi ndani ya nyumba ya Masoeurs.

**2014**
Tulianza mwaka na Mapadri walewale, lakini tulipokua katika mkutano mkubwa pa Bukavu mwezi wa kwanza, Padri mkubwa na msimamizi wa Mapadri jimboni, Padri Faustin Turco alitueleza ya kama ku Paska kutakuwa mabadiriko ndani ya jamaa la Mapadri wa Kitutu.


Butetegele, 2008

Tarehe 19/02/2014, tunawapokea Mapadri wapya: Bernard Cibambo, na Hieronimus Harum.

Don Antonio pamoja na Baba yake wakaondoka na kwenda kubaki Uvira huko alikochaguliwa na Baba Askofu kuwa mlinda Azina wa jimbo la Uvira.
Tarehe 18/03, kufuatana na matangazo ya Papa Fransisko na Askofu wetu Sébastien, tulianza kufikiri na kusali kuhusu jamaa na kuanza *Mwaka wa jamaa*.
Tukio kubwa ni kumpokea mara ya kwanza akina Baba askofu Sébastien Muyengo Mulombe. Tarehe 04 mpaka 07/04/2014, katika safari yake ndani ya Parokia, alisimama ndani ya kila Diakonia ya secteur nord, na kusoma Misa kubwa pa Sugulu. Alikuwa akisindikizwa na Vicaire général Milenge Flavien na ujumbe mkubwa wa mapadri na wengine wa Laics.
Pa Kitutu, alisoma Misa, na katika misa hiyo alibariki waongozi wapya.
Tarehe 22/04/2014, Padri Augustino anaenda likizo (*Congé*) kwao na hakurudi tena. Kiisha karibuni mwaka moja, walaiques consacrés (Christine na Marie Jeanne) walituacha na kurudi Bukavu.


Byonga, 2008

Katika mwaka huu ndani ya jimbo letu kuliundwa "tume" mbalimbali za Eklezia. Mwezi wa tano, tume hizo zimesimikwa katika Parokia. Kwa ngambo ya maendeleo, Mapadri walianza ukarabati na majengo ya vyumba vingine vipya vya kituo cha afya Busakizi, na tarehe 26/12/2014 chumba cha kuzalia kikafunguliwa.

**2015**
Mapadri ni watatu: P. Codutti Gianpaolo, P. Bernard Cibambo na P. Hieronimus Harum.
Sababu ya uchelevi, tuliendelea kwa mwaka huu kupana mafundisho wakati wa kwarezyma na Paska kwa kila secteur kuhusu *Jamaa*. Mwaka huu tulijenga lupango inayo linda nyumba ya Masoeurs na kusafisha vyumba vimoja ndani ya nyumba ile.
Mwezi wa nane, tangu tarehe 19 mpaka 21, Askofu alitutembelea, kwa mda fupi kwani alikuwa katika matembezi pa Mwenga na Kamituga. Kwetu, Askofu alitembelea Diakonia ya Mela, hapo alisoma Misa kwa ajili ya wakristu wote wa secteur ya *bassin d'Elila*. Ilipo fika mwezi wa

kenda tarehe 03, tulipokea mséminariste moja wa Waxaveriano kwa stage, Christophe Ndiwe Chiza.
Tarehe 08 mpaka 12, kufuatana na mpango wa Papa Fransisko tulianza mwaka wa pekee wa huruma ya Bwana, uliofunguliwa na Misa kubwa. Kila Diakonia alipokea barua ya Askofu *Muwe na huruma kama vile baba wenu alivyo na huruma* iliyo sindikizwa na fikara mbalimbali kwa kusaidia kuishi neno la Mungu. Mda wa majilio, tulisaidiwa na Mapadri: Faustin Turco, Gerardo Pretel na Willy Nkumbo.
Kama kawaida, tunawapokea mwezi wa saba waséminaristes waxaveriano: pamoja na vijana wanaojitolea kwa kuongoza watoto mda wa mafungo, yaani *Colonie des Vacances*.



Jubilée d'or du Diocèse, Kitutu 27.05.2012

**Wengi sana walitangaza Habari Njema kwa njia ya nyimbo na ya utumishi katika ibada !**

## 6. HADISI FUPI YA DIAKONIA ZETU



Kibe, 2008

### 1. Diakonia ya Kibe

Diakonia ya Kibe ilianza mwaka wa 1993. Mwongozi wa kwanza aliitwa Kilosho Lungele. Ngambo ya maendeleo: kanisa moja ya tofali ama jengo la kudumu, gîte na choo la kudumu.

### 2. Diakonia ya Makito



Makito, 2008

Ilianza kuwa diakonia mwaka wa 2001, tarehe 23 mwezi wa kumi na mbili. Mwongozi wa kwanza alikuwa Wasolu André na makamo wake Bitesi Jean-Marie-Vianney.
Ngambo ya maendeleo: tunayo kanisa, bureau na gîte, majengo ya kudumu. Ngambo ya masomo, tuna masomo ya msingi na ya secondari.

### 3. Diakonia ya Sugulu

Diakonia hii imepata misingi yake ndani ya Diakonia ya Mitobo, mwaka wa 1983. Mitobo iligawanyika na kuunda Diakonia ya Sugulu.
Mwongozi wa kwanza alikuwa Kasindi Dunia Erneste. Ngambo ya maendeleo, tunayo kanisa kubwa lenye jengo la kudumu, gîte, bureau na

chumba cha mikutano. Tunayo pia masomo ya msingi na ya secondari, yote imejengwa kwa vifaa vya kudumu.

**4. Diakonia ya Mitobo**

Diakonia ya Mitobo ilianza tarehe 24/09/1969. Mwongozi wa kwanza alikuwa Byabele Dismas. Kwa ngambo ya maendendeleo, tuna kanisa lenye jengo la kudumu, masomo ya msingi na ya kisecondari, chumba cha vijana pia wanja la kabumbu.

**5. Diakonia ya Milima**

Diakonia hii ilianza mwaka wa 1992. Mwongozi wa kwanza alikuwa Mateso Musiwa Aurélien. Ngambo ya maendeleo: kanisa na masomo ya msingi ya kudumu.

**6. Diakonia ya Maka**

Mbele ya Kitutu kupata Parokia kwa mwaka 1967, Maka ilikuwa kijiji cha Parokia ya Kamituga. Parokia ilipofika Kitutu, Maka ikapewa Centre ya Ibada. Mwaka wa 1995, Maka ikageuka kuwa Diakonia. Mwongozi wake wa kwanza ni Mulonda Ombeni Martin. Kwa ngambo ya maendeleo, tunayo sasa ujenzi wa Kanisa. Kwa leo Wakristu karibu wote walihamia Kitutu, hata masomo ya msingi imehamia Kitutu.

**7. Diakonia Kazuza**

Diakonia hii ilianza mwaka wa 1972 na mwongozi wa kwanza aliitwa Itulamya Baltasard.

Kwa ngambo ya maendeleo, tunayo masomo ya msingi na Kanisa la kudumu.

**8. Diakonia ya Tukenga**

Mbele ya kuwa Diakonia, ilikuwa Centre ya Ibada ya Diakonia ya Kazuza. Mwaka wa 1990, Tukenga ikatajwa kuwa Diakonia na Mwongozi wa Kwanza aliitwa Itongo Wakenge. Kwa ngambo ya maendeleo, tunayo kanisa moja la



Tukenga, 2008

kudumu na chumba moja ya mikutano ya kudumu. Tena tuna masomo ya msingi yenye darasa tano ya kudumu na nne ya miti.

**9. Diakonia ya Kagelagela**

Diakonia hii ilikuwa kijiji cha Diakonia ya Kazuza. Munamo mwaka wa 1997, Kagelagela iligeuka kuwa Diakonia. Mwongozi wa kwanza aliitwa Mulonda Mbaluku Dieudonné. Ngambo ya maendeleo: tupo katika majengo ya kanisa (majengo ya kudumu). Tuna masomo ya msingi ila kwa udongo.

**10. Diakonia ya Itula**

Diakonia hiyo, ilianza mwaka wa 1972 na Mwongozi wake wa kwanza aliitwa Mulombe wa Lugezi Désiré. Kwa ngambo ya maendeleo, tupo na kanisa moja, majengo ya kudumu na masomo ya msingi pia masomo ya secondari ya kudumu. Diakonia ilijinunulia pia machine moja ya kuponda matofari.

**11. Diakonia ya Zingu**

Diakonia hii ilianza mwaka wa 1976, na Mwongozi wa kwanza aliitwa Kikuni Adolphe. Kwa ngambo ya maendeleo, diakonia ya Zingu inayo Kanisa moja la kudumu. Tupo pia katika majengo ya masomo ya secondari.

**12. Diakonia ya Kitindi**

Diakonia hii ilitangazwa na Padri Paulo Maran tarehe 23/09/2007. Mwongozi wa kwanza aliitwa Makindu Gilbert. Kwa ngambo ya maendeleo, kanisa la Diakonia linajengwa na matofali; tunayo masomo tatu ya msingi (ya Katete, Nkoba na Lukwaza).

Kwa leo, tupo na ponda matofali kwa ajili ya majengo nyipya ya masomo na kanisa.



Mela, 2008

**13. Diakonia ya Mela**

Mela ilitajwa kuwa Diakonia na Padri Pino Rizzi, munamo tarehe 10/03/2002.

Mwongozi wake wa kwanza aliitwa Fataki Kise. Kwa ngambo ya maendeleo, tunayo kanisa moja ya kudumu, bila pavement. Tunayo pia somo la msingi, ila somo nne tu ndiyo la kudumu.

### 14. Diakonia ya Kakemenge

Diakonia hii ilianza tangu tarehe 01/06/1973. Mwongozi wa kwanza aliitwa Kibiswa Lulelwa. Kwa ngambo ya maendeleo, tumejenga kanisa kubwa la matofali na tunaendelea kuponda matofali kwa kutengeneza chumba cha kusomea, kilicho bomoka. Tunayo vyumba vya katekezi. Tunayo masomo ya msingi ambayo tupo na ponda matofali kwa kujenga somo tatu zilizo baki.

### 15. Diakonia ya Lugushwa

Diakonia hii ilianza tangu mwaka wa 1967. Mwongozi wake wa kwanza aliitwa Basubi Prospère. Kwa ngambo ya maendeleo, diakonia lina jengo la kudumu, lina gîte ya Mapadri. Tunayo mashirika 12 yenye kujengwa na matofali. Katika Diakonia ya Lugushwa, tunazo masomo matatu ya msingi isiyojengwa na matofali na somo moja ya secondari iliyojengwa na matofali.



Mapale, 2008

### 16. Diaconia ya Bonde

Diakonia hii ilizaliwa na Diakonia ya Lugushwa, munamo tarehe 27/11/1984. Mwongozi wa kwanza alikuwa Batibuka Gabriel. Kwa ngambo ya maendeleo, tunayo kanisa ya kudumu pia masomo ya msingi bado kujengwa kwa matofali.

### 17. Diakonia ya Butetegele

Ilianzishwa mwaka wa 2000. Mwongozi wake wa kwanza alikuwa Kisege Mukamba Alexis. Kwa ngambo ya maendeleo, tupo na kanisa moja ya matofali, pia tunayo masomo ya msingi.

### 18. Diakonia ya Kabikokole



Kabikokole, 2008

Ilianzaitwa Diakonia mwaka wa 1995. Mwongozi wa kwanza aliitwa Kikukama Wakeka Rogatien. Kwa ngambo ya maendeleo, tupo na jenga kanisa kubwa la matofali.

### 19. Diakonia ya Iwiwi



Mbele ya kuwa Diakonia, ilikuwa kijiji cha Diakonia ya Tukenga. Katika mwaka wa 2001, Iwiwi ikatajwa kuwa Diakonia, Mwongozi wa kwanza aliitwa Mutumoyi Banamwezi Justin.



**Shukrani kwa waongozi, wasimamizi na wakatekista wote wa Kitutu!**

Hapa ni marehemu Wabesha Eugène, mwongozi makamo ya Kitutu (mwanzo wa miaka 2000).

# 7. WAXAVERIANO NA ABBÉ WALIOKUWA KITUTU

| | | | |
|---|---|---|---|
| 1  | 2  | 3  | 4  |
| 5  | 6  | 7  | 8  |
| 9  | 10  | 11  | 12  |
| 13  | 14  | 15  | 16  |
| 17  | 1. Arrigoni P. Giuseppe, 2. Berton P. Angelo, 3. Chiminazzo P. Attilio, 4. Marangoni P. Ezio, 5. Noris P. Italo, 6. Camorani P. Lorenzo, 7. Ferrari Fr. Angelo, 8. Querzani P. Graziello, 9. Ballarin P. Lino,10. Rottini P. Aldo, 11. Nardo P. Riccardo, 12. De Mattia P. Pio, 13. Benedetti P. Silvano, 14. Dovigo P. Giuseppino, 15. Grigis P. Evasio, 16. Colasuonno P. Nicola, 17. Cisco P. Giuseppe | | |

| | | | |
|---|---|---|---|
| 18  | 19  | 20  | 21  |
| 22  | 23  | 24  | 25  |
| 26  | 27  | 28  | 29  |
| 30  | 31  | 32  | 33  |
| 34  | 18. Agostini P. Piergiorgio, 19. Da Rold P. Sisto, 20. Raffaini P. Fiorenzo, 21. Valenti P. Giampietro, 22. Bon P. Renzo, 23. Marconi P. Dino, 24. Agostinis Pierfrancesco, 25. Festa P. Mario, 26. Tomasi P. Natalino, 27. Manzotti P. Antonino, 28. Rizzi P. Giuseppe, 29. Galli P. Giuseppe, 30. Sciamanna P. Mario, 31. Turco P. Faustin, 32. Maran P. Paolo, 33. Rinaldi P. Pietro, 34. Jimenez Serrano P. Guillermo | | |

| | | | |
|---|---|---|---|
| 35  | 36  | 37  | 38  |
| 39  | 40  | 41  | 42  |
| 43  | 44  | 45  | |

35. Mendoza Silva P. Roberto Carlos, 36. Simoncelli P. Giulio, 37. Olvera Gonzalez P. José Pedro, 38. Codutti P. Gianpaolo, 39. Pretel Ortiz P. Gerardo Ernesto, 40. Gonzalez Angulo P. Augustin Jaime, 41. Romano P. Antonio, 42. Cibambo Rubibi P. Bernard, 43. Harum P. Hieronimus, 44. Ndiwe Chiza Christophe, 45.Shadari Tutu P. Paulin

## 8. KWA KUMALIZA

Tunamshukuru Mungu kwa yote aliyotutendea katika Parokia yetu.
Kwa Mapadri na Frera wote waliotumika na kujitolea kwa maendeleo ya hapa kwetu Kitutu (wamoja wakiwa hai na wengine wamekwisha fariki).
Kwa Waongozi wote waliokubali kutumika kwa maendeleo ya Eklezya na ya nchi, Wakatekista, Wasimamizi wa Mashirika na vikundi vya Eklezya bila kusahahu Waalimu wa Masomo na Directeur yao.
Mda wa miaka hii yote, tumepata Mapadri wazaliwa wa Kitutu:

P. Katindi Ramazani Alphonse, Xaveriano.
P. Muganza Musimbi Deogratias, Xaveriano (aliacha upadri)
Abbé Lwesso Mwanga Boniface (aliacha upadri)
Abbé Zakalamo Luusu Polydore
P. Bulambo Barthélémy, Franciscain.
Abbé Mulonda Kyatogekwa Joseph

Tulipata Masoeurs wawili wa *Compagnie de Marie*:

Sr Anna Musingwa
Sr Symphorose Kasindi (aliyefariki pa Kinshasa, tarehe 06/10/2016)


Tunao pia Waséminaristes wakubwa wanaojitayarisha kupokea Upadirisho:

Mulonda Lweku Jean-Baptiste
Alamo Pona Dominique

Kunako Propédeutique, tunao vijana tatu; katika *Petit Séminaire* ya Mungombe kuna watoto 4 ya Kitutu.
Hawa wote ni matunda ya Parokia yetu.

*Mavuno ni mengi, wafanya kazi ni wachache,*
*tuma Bwana watumishi wengine shambani mwako*

# Daftari ya maparoko ya Kitutu

| | | | |
|---|---|---|---|
| 1  | 2  | 3  | 4  |
| 5  | 6  | 7  | 8  |
| 9  | 10  | 11  | 12  |
| 13  | 14  | 15  | 16  |
| 17  | 1. Arrigoni (67-70), 2. Chiminazzo (70-71), 3. Camorani (71-73), 4. Chiminazzo (73-76), 5. Dovigo (76-81), 6. Grigis (81-84), 7. Colasuonno (84-86), 8. Da Rold (86-88), 9 Agostini (89-93), 10. Benedetti (93-95), 11. Bon (95-96), 12. Festa (96-97), 13. Tomasi (97-99), 14. Rizzi (99-04), 15. Festa (04-05), 16. Maran (05-09), 17. Codutti (tangu 2009) | | |